# LEARNING BY EAR

## Lent Luxury-The risks of raising credit

## EPISODE SIX: THE GUARANTOR & COLLATERAL RISK

**AUTHOR: JAMES MUHANDO**

**EDITORS: Adrian Kriesch, Friederike Müller**

**PROOFREADER: Tony Dunham**

**Kisuaheli: Eric Ponda**

**LIST OF CHARACTERS BY SCENE:**

**SCENE ONE AT GIDDY'S.**

- **NARRATOR (M 30)**
- **UNCLE BARRY(M 45)**
- **ZILPAH (F 35)**
- **LUCIA (F 11)**
- **Giddy (M15)**

**SCENE TWO:AT JD'S.**

- **ZILPAH (F 35)**
- **NINA (F 35)**
- **GIDDY (M 15)**
- **NARRATOR (M 30)**

**SCENE THREE: AT THE DINNER TABLE.**

- **LUCIA (F 11)**
- **GIDDY (M 15)**
- **ZILPAH (F 35)**
- **THUG 1 (M 40’S)**
- **THUG 2 (M 40’S)**
- **NARRATOR (M 30)**

**SCENE FOUR: IN THE POLICEMAN’S OFFICE.**

- **MAMA JENNY (F MID 30’S)**
- **OFFICER (M 50)**
- **JENNY (F 15)**
- **SECRETARY (F MID 20’S)**

  **ZILPAH (F 35)**
- **NARRATOR (M 30)**

**SCENE FIVE: ON THE WAY BACK FROM THE POLICE STATION IN THE AFTERNOON.**

- **NARRATOR (M 30)**
- **MAMA JENNY (F MID 30’S)**
- **ZILPAH (F 35)**
- **NINA (F 35)**

- **JENNY (F 15)**
- **JD (M 15)**
- **GIDDY (M 15)**

**INTRO:**

**1. ATMO: OFFICE AMBIENCE**

**2. SFX: DOOR OPENS,FOOTSTEPS**

**3. NARRATOR:**

Hujambo msikilizaji na kwa mara nyingine tena katika ofisi yangu tuendelee na mfululizo wa vipindi vya Noa Bongo jenga maisha yako kwenye mchezo wa Redio Starehe za Kuazima -Tatizo la kulipa mkopo. Bila shaka bado unanikumbuka jina langu Gideon Leboo. Mimi ndiye mhusika mkuu katika hadithi hii na pia mmoja wa wafanyakazi katika benki. Nitaendelea na hadithi kuhusu ujana wangu. Bila shaka katika kipindi kilichotangulia, rafiki yangu JD anafikishwa katika kituo cha polisi na babake baada ya babake kufahamu ulaghai alioutenda wa kughushi sahihi yake ili aweze kupata mkopo wa baiskeli. Naye Jenny anavunjika mkono tukijaribu kumtoroka Gori aliyetukopesha pesa na kushindwa kumlipa. Sikuweza kwenda nyumbani kwa sababu niliwaona watu wawili nje ya nyumba yetu ambao nilishuku tabia zao. Hivyo usiku kucha nilikesha kwenye zizi la ng'ombe (**Laughs**). Lakini wakati nilipoingia nyumbani asubuhi hiyo, mambo niliyokutana nayo hayakuwa ya kufurahisha hata kidogo.

**SCENE ONE: AT GIDDY'S**

**4. ATMO: INSIDE GIDDY'S HOME**

**5. UNCLE BARRY:** Habari Giddy! Umefika! Sijakuona kwa siku nyingi, hebu pita ndani umsalimie mjomba Barry. Uko hapa. **(To Zilpah)** Zilpah! Kijana amefika!

**6. SFX: RUNNING FOOTSTEPS AS ZILPAH APPROACHES.**

**7. ZILPAH: (Happily)** Oh mtoto wangu! Giddy uko salama? Nimekuwa nikikuwaza sana. Na nusra nipoteze maisha kwa kuhofia maisha yako!

**8. SFX: HUGS HIM.**

**9. ZILPAH:** Na ni harufu ya nini hiyo nasikia? **(Pause)** Lucia, wewe umesimama tu hapo badala ya kumtengenezea chai kakako. Huoni baridi imempata.

**10. LUCIA: (Ironically)** Oh, makini kijana… **(Pause, then the she decides to spill the beans)** Mama, Giddy na rafiki zake waliiba redio ya mjomba Barry!

**11. ZILPAH: (Shocked)** Eti nini?

**12. NARRATOR:**

Maskini kijana mtundu. Kisha usoni pa mjomba Barry mwenye redio ambayo iliwekwa dhamana kwa Bw. Gori ili JD aweze kupata mkopo! Sikujua kwamba mjomba Barry angetokezea ghafla baada ya kutoweka miaka yote hiyo. Kisha nikalazimika kuelezea hadithi yote. Pia ilinibidi nizungumzie kisa cha majambazi wawili niliyokutana nao nje ya nyumba yetu. Na kushangaa iwapo mjomba Barry aliwaona alipokuwa akiwasili nyumbani. Lakini kumbe hakuwa amewaona! Walikuwa kina nani, nilizidi kujiuliza maswali huku mamangu akinivuta masikio kunipeleka nyumbani kwa kina JD.

**<u>SCENE TWO: AT JD'S.</u>**

**13. ATMO: OUTSIDE, COW'S MOOING, MORNING AMBIENCE IN THE VILLAGE.**

**14. SFX: SOUND OF MILK SQUIRTING INTO A CONTAINER AS SHE MILKS.**

**15. SFX: FOOTSTEPS (2 PEOPLE) APPROACHING.**

**16. ZILPAH: (Shouts)** Nina!

**17. NINA:** Zilpah! Umeamka mapema leo. Na hata wewe Giddy pia. Si leo ni Jumamosi?

**18. ZILPAH: (Unfriendly)** Unajua kwamba mtoto wako sasa ni kiongozi wa genge la majambazi?

***KW begin***

**19. NINA: (Confused)** Mtoto wangu? Kiongozi wa genge la majambazi? Una maana gani?

**20. ZILPAH:** Mtoto wako ndio mhusika mkuu wa njama kuhusu mambo yanayoendelea katika kijiji hiki, Nina!

***KW end***

**21. NINA: (Bewildered)** Unasema nini?

**22. ZILPAH:** Nazungumza kuhusu JD JD! Cha kushangaza amemshawishi kijana wangu alivyo mpumbavu kwenda wakivunja nyumba za watu na kuiba mali!

**23. GIDDY:** Sikusema hi...

**24. ZILPAH: (Slaps him)** Nyamaza! Hebu mwambie yote uliyonielezea. Tena sasa hivi!

**25. NARRATOR:**

Nilimueleza mamake JD yote yaliyotokea kuanzia mwanzo. Lakini kama nilifikiri kuwa mamangu ndiye aliyekasirika zaidi, nilikuwa najidanganya tu! Mamake JD alishikwa na wazimu zaidi na hangesubiri kumuadhibu JD! Lakini JD alikuwa akisikia yote tuliyokuwa tukizungumza na wakati mamake alipofika chumbani tayari JD alikuwa ametoroka.

Leo usiku, mjomba Barry anafika nyumbani akitokwa na damu puani. Akisema kwamba ameanguka shimoni, lakini nilijua ni uongo. Siku iliyofuata alikuwa ametoweka. Na baadaye, tukaja kugundua kwamba alikuwa ametoroka na baadhi ya vitu nyumbani …

**<u>SCENE THREE: AT DINNER</u>**

**26. ATMO: NIGHT SOUNDS, CRICKETS. AT GIDDY’S**

**27. SFX: CUTLERY AS PEOPLE EAT.**

**28. LUCIA: (Whispers to Giddy)** Samahani sana Giddy!

**29. GIDDY:** Usizungumze na mimi!

**30. LUCIA:** Lakini nakuomba msamaha!

**31. GIDDY: (A bit loud)** Niache!

**32. ZILPAH: (Firmly)** Wewe! Kula!

**33. SFX: SILENCE, CUTLERY.**

34. **ZILPAH:** Una uhakika ulimuona mjombako akitoka na mkoba Lucia?

35. **LUCIA:** Ndio. Lakini yeye hakuniona! Mimi nilichungulia kwa dirishani na nikamuona akibeba mkoba.

36. **GIDDY:** Ni kweli kazi yako ni kuchunguza watu tu!

37. **ZILPAH:** Tosha, tosha Giddy! **(Pause)** Sijui ni kwanini mjombako ameondoka bila ya kutuaga.

38. **SFX:** **KNOCK ON THE DOOR.**

39. **ZILPAH:** **(Calls)** Huyo ni Barnabas?

40. **THUG 1:** **FROM OUTSIDE**

**(Clears his throat, pretends to be Uncle Barry)** Yes.

41. **ZILPAH:** Gideon, mfungulie mjombako.

42. **SFX:** **FOOTSTEPS, DOOR OPENS.**

43. **SFX:** **COMMOTION AS THUGS PUSH GIDDY IN.**

44. **GIDDY:** **(Screams)**

45. **THUGS:** **(Menacingly)** Rudi ndani haraka! Na kila mmoja alale chini!

46. **ZILPAH/LUCIA:** **(Scream)**

47. **THUG 2:** Kimya kila mmoja. Mkinyamaza hakuna kitu kitakachomtokea! Yuko wapi?

48. **ZILPAH:** **(Panicked)** Nani? Nani yuko wapi?

**49. THUG 1:** Unafahamu tunamuliizia nani, John Mark, yuko wapi? Na usijaribu kutudanganya, kwani tulimuona hapa jana usiku!

**50. ZILPAH:** Hatumjui mtu anayeitwa John Mark!

**51. THUG 2:** Mama, Chunga mdomo wako, kabla ya kuzungumza na mimi. Hujui unaongea na nani. Humjui huyu mtu kwenye picha hii?

**52. LUCIA:** **(Innocently)** Huyo si John Mark. Ni mjomba Barry!

**53. THUG 2:** Na yuko wapi?

**54. LUCIA:** Ameondoka asubuhi na mapema leo. Amerudi jijini!

**55. THUG 2:** Unatudanganya sisi wewe msichana? **(to Thug 2)** Soja!

**56. THUG 1:** Naam, Masta!

**57. THUG 2:** Kagua hivyo vyumba!

**58. SFX:** **SOUNDS OF MOVING FURNITURE,**

**THUG 1 WALKS THROUGH THE HOUSE**

**59. THUG 1:** **(Calls)** Hayupo hapa!

**60. THUG 2:** Na hiyo mali?

**61. THUG1:** Pia siioni!

**62. THUG 2:** **(To Zilpah)** Uko wapi?

**63. ZILPAH:** Nini?

**64. THUG 1:** Iko wapi hati miliki ya shamba ambayo .. eeh mjomba Barry aliahidi kuiwasilisha kwetu kulipa mkopo aliochukua kutoka kwa mkubwa wetu?

**65. NARRATOR:**

Majambazi hao walipekua kila pembe ya nyumba hiyo lakini wapi, hawakupata kile walichokuwa wakitafuta. Wakatuambia mjomba Barry alikuwa ameahidi kuwasilisha hatimiliki ya shamba kama dhamana kwa mkopo aliokuwa amechukua kutoka kwa mkubwa wa benki. Mamangu alishangaa sana. Hati hiyo ilionyesha kuwa mamangu ndiye mmiliki halali wa shamba letu. Isitoshe akawaambia wachakure kila mahali kwenye makabati chini ya kitanda lakini hawakupata chochote. Baadaye Lucia akasema kuwa alimuona mjomba Barry akitoa bahasha ya rangi ya udhurungi kutoka kwenye kabati. Na kisha majambazi hao wakatoa haraka hao! Lakini tayari mamangu alikuwa amepoteza hati ya kumiliki shamba, sawa na kupoteza shamba zima. Kwani hatimiliki hiyo ndiyo iliyokuwa ngao ya maisha yake. Baadaye asubuhi hiyo akaenda moja kwa moja kuripoti kisa hicho kwa polisi. Lakini akashangaa kwamba hakuwa peke yake.

**SCENE FOUR: AT THE POLICE STATION.**

**66. OFFICER:** Mama Jenny, nimekwambia tunafanya kila juhudi kumsaka Gori. Tutakwambia punde tu tutakapomkamata.

***KW begin***

**67. MAMA JENNY:** Lakini inachukua muda sana Bw. Ofisa.

**68. OFFICER:** Tumepata habari kwamba amejificha huko kijijini. Punde tu tutakapopata uhakika wa habari hizo tutakwenda kumkamata.

***KW end***

**69. MAMA JENNY:** Lakini je mtawachukulia hatua gani vijana waliosababisha haya yote?

**70. OFFICER:** Napanga kuwatembelea Luka na Zilpah leo asubuhi. Lakini huwezi kuwalaumu vijana. Hata huyu binti yako pia alihusika pakubwa katika kisa hicho.

**71. MAMA JENNY:** Jenny alidanganywa tu afisa, na kisha mimi ndiye niliyegharamia matibabu yake hospitalini!

**72. SFX: SOFT KNOCK ON THE DOOR.**

**73. SECRETARY:** Samahani kwa kukukatizia, afisa lakini kuna mtu anataka kuzungumza na wewe hapa.

**74. OFFICER:** Lakini huoni niko na shughuli nafanya? Ni nani huyo?

**75. SECRETARY:** Anasema ni dharura. Jina lake ni Zilpah.

**76. OFFICER:** Zilpah? Huyu mwanamke ninayemtafuta. Mruhusu angie.

**77. SFX: FOOTSTEPS.**

**78. ZILPAH:** Habari ya asubuhi afisa. Oh, Jenny? Kumbe pia wewe uko hapa? Nimesikia yote yaliyotokea. Pole sana. Umetoka lini hospitanini.

**79. JENNY:** Jana tu Mama Giddy.

**80. MAMA JENNY: (Moodily)** Mbona hukushughulika hata kwenda kumtazama hospitalini? Na kisha mtoto wako ndiye aliyesababisha mambo yote haya, Zilpah?

***KW begin***

**81. ZILPAH:** Samahani? Na ni vipi mtoto wangu alisababisha vipi mambo haya Mama Jenny?

**82. MAMA JENNY:** Ni mtoto wako aliyekwenda kukopa pesa kutoka kwa yule mlaghai Gori......

***KW end***

**83. ZILPAH: (Cuts in)** Una uhakika ya unayoyasema! Ni mtoto wa Nina na wala si mtoto wangu aliyekwenda kukopa pesa kutoka kwa Gori!

***KW begin***

**84. OFFICER:** Sawa! Tosha, tosha !

**85. MAMA JENNY:** Hapana ofisa. Huyu mwanamke lazima anisaidie kugharamia matibabu ya binti yangu hospitalini!

**86. ZILPAH:** Na kwanini unamuita mwanamke?

**87. MAMA JENNY:** Wewe! Nani mwengine...

***KW end***

**88. OFFICER: (Authority)** Tosha! tosha **(Pause)** Naona kuna kesi nyingi hapa. Nataka vijana nyote watatu mfike ofisini kwangu leo mchana mkiwa mmeandamana na wazazi wenu. Ehhe, nini kilichokuleta hapa Zilpah?

**89. ZILPAH: (Sighs)** Tulivamia jana usiku.

**90. NARRATOR:**

Mara moja maafisa hao wa polisi walianzisha msako mkali na kufikia jioni walikuwa wamewatia mbaroni majambazi wawili waliokuwa wamejificha katika hoteli moja kijijini. Alifikiria ni miongoni mwa majambazi waliokuwa wametumwa na Gori, lakini baada ya kuhojiwa wakakiri kuwa walikuwa wametumwa kutoka mjini kuja kudai pesa kutoka kwa mjomba Barry. Maafisa hao wa polisi waliwakamata kwa kuingia katika nyumba ya mtu bila ya idhini. Wakati wa mchana, mimi, JD na Jenny pamoja na wazazi wetu tulifika kitu cha polisi, huku tukiagizwa turipoti kila asubuhi katika kituo hicho ambako tuliulizwa maswali hayo hayo kila siku !

Mimi nilishtakiwa kwa kuiba redio ya mjombangu, JD kwa kosa la udanganyifu kwa kughushi sahihi ya babake naye Jenny kwa kusaidia na kuficha uhalifu. Wakati wote wazazi wetu walikuwa kimya hadi pale Mama Jenny alipovunja kimya hicho.

**SCENE FIVE: ON THE WAY BACK FROM THE POLICE STATION IN THE AFTERNOON.**

**91. ATMO: RURAL ROAD.**

**92. SFX: FOOTSTEPS.**

**93. MAMA JENNY:** Zilpah, samahani sana kwa nilivyokufokea asubuhi.

**94. ZILPAH:** Usijali Mama Jenny.

**95. MAMA JENNY:** Mara nyingine watoto wanaweza kukuaibisha.

**96. NINA:** Naona aibu sana kwa aliyofanya mwanangu JD.

***KW begin***

**97. MAMA JENNY:** Na kisha tunawafunza kila siku. Au mimi sijakufunza jinsi na umuhimu wa kuweka akiba Jenny?

**98. JENNY:** Umenifunza mama.

**99. ZILPAH:** Na wewe Giddy, nimekwambia mara ngapi daima usijilinganishe na maisha ya watu wengine, au sijakwambia hivyo?

**100. GIDDY:** Umeniambia.

**101. ZILPAH:** Kisha tatizo ni gani?

**102. SILENCE**

**103. NINA:** Usiwalaumu. Mlaumu huyu kijana wangu mjinga.

***KW end***

**104. MAMA JENNY:** Nafkiri bora tuwafunze watoto wetu jinsi ya kuweka akiba. Ni muhimu sana kuweka akiba sehemu ya pesa unazopata. Ikiwa utaweza kuweka akiba zaidi na kubana matumizi, basi si rahisi kwenda kuchukua mkopo. Sawa watoto?

**105. GIDDY/JD/JENNY:** Ndio mama/ ndio mama Jenny!

**<u>OUTRO</u>:**

**106. SFX: OFFICE ATMO**

**107. NARRATOR:**

(Sights) Chakusikitisha ni kwamba vijana kote barani Afrika wanakumbwa na matatizo sawa.

Kila mmoja anataka kuwa na simu ya bei ghali, Komputa mpya na mavazi ya kisasa kabisa. Lakini kama kuna jambo muhimu zaidi nimejifunza katika ujana wangu na hata hapa kazini, ni bora kujifunza kuishi kadri ya uwezo wako. Unajitia mashakani pale unapoanza kujilazimisha maisha ambayo huwezi kuyamudu.

Hadi kufikia hapo msikilizaji tunafika mwisho wa makala haya ili nami nipate nafasi ya kurudi kazini. Kwa mengi zaidi ungana nasi katika kipindi kinachofuata ili uweze kujifunza mengi zaidi. Endapo ungependa kukisikiliza tena kipindi hiki

basi tembelea mtandao wetu wa: dw.de/lbe, na pia ukiwa na maoni usisite kututumia kupitia ukurasa wetu wa Facebook. Na kama nilivyokuahidi usikose kuungana nasi tena usikie kitakachotokea kwa Gori na mjomba Barry. Asanteni kwa kutusikiliza hadi wakati mwengine. Kwaheri kwa sasa.

.